



SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

6 Barabara ya Health Office
Mnazi Mmoja S.L.P 236
70467 Milni Maoharibi -Zanzibar

WIZARA YA AFYA

Tovuti: www.mohz.go.tz
Barua pepe: info@mohz.go.tz

TAREHE 19 Agosti, 2024

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU TAHADHARI YA UGONJWA WA HOMA YA NYANI (MONKEYPOX)

Wizara ya Afya imepokea taarifa ya kuwepo kwa ugonjwa wa Homa ya Nyani kutika nchi jirani ya Kenya. Ugonjwa huu unasababishwa na virusi aina ya *monkeypox*, kutoka familia ya virusi vya *smallpox*. Awali maambukizi yalianza kutoka kwa wanyama kwenda kwa wanadamu, hasa katika nchi zilizo karibu na misitu ya mvua ya kitropiki.

Hadi sasa, hakuna mgonjwa yoyote wa Homa ya Nyani aliyethibitishwa hapa Zanzibar na Tanzania kwa jumla, hata hivyo, tahadhari zimewekwa ili kuhakikisha ugonjwa huo hauingii nchini. Dalili za Homa ya Nyani ni pamoja na homa, maumivu ya kichwa, misuli, mgongo, uchovu, na kuvimba mitoki, upele, malengelenge, au vidonda vinaweza kutokea kwenye mwili, kwa kawaida huchukua wiki mbili hadi nne.

Kulingana na takwimu za hivi karibuni, kumekuwa na jumla ya visa 38,465 na vifo 1,456 vimetiwa tangu Januari 2022 hadi Julai 2024 katika bara la Afrika. Virusi vya Homa ya Nyani vinaenea kwa kasi, hasa katika nchi za Afrika Magharibi na Kati ambapo ugonjwa huo umeripotiwa kusambaa katika nchi 15 Barani Afrika, wataalamu wameona kuwa hali inaweza kuwa mbaya zaidi kama hatua za haraka hazitachukuliwa.

Ingawa hakuna kisa chochote cha ugonjwa huo kilichoripotiwa hapa Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanza kuchukua hatua za tahadhari dhidi ya ugonjwa wa Homa ya Nyani (Mpox) hasa kwa vile kumeripotiwa ongezeko la maambukizi ya ugonjwa huo katika nchi jirani za Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Wizara imeimarisha mifumo yake ya ufuatiliaji wa magonjwa (Disease surveillance) hasa katika viwanja vya ndege na bandari kwa kuimarisha uchunguzi wa afya kwa wasafiri wanaoingia nchini, kutoa mafunzo kwa wahudumu wa afya juu ya kutambua, kutoa huduma pamoja kujikinga na ugonjwa huo, kutoa elimu kwa wananchi kuchukua hatua na kujikinga dhidi ya ugonjwa wa Homa ya Nyani na kuhakikisha vifaa tiba na kinga vipo maeneo ya kutolea huduma.

Wizara ya Afya inawaomba wananchi wote wa Zanzibar kuhakikisha nchi yetu inabaki kuwa salama kwa kuchukua hatua za kujikinga na ugonjwa huu kwa kutekeleza yafuatayo:-

- i. Kutoa taarifa kwa kupiga simu namba 190 bila malipo endapo utamuona mtu mwenye dalili za ugonjwa Homa ya Nyani.
- ii. Kuepuka kugusa majimaji ya mwili au ngozi ya mtu mwenye dalili za ugonjwa
- iii. Kuepuka kugusana na mtu yeyote mwenye dalili za ugonjwa wa Homa ya Nyani..

- iv. Kunawa mikono kila mara kwa maji tiririka na sabuni au kutumia vitakasa mikono.
- v. Safisha na kutakasa vyombo vilivyotumika na mhisiwa au mgonjwa pamoja na maeneo yote yanayoguswa mara kwa mara.
- vi. Kuvaa barakoa iwapo itabidi kukaa na kuongea kwa karibu na mtu mwenye dalili za Homa ya Nyani.
- vii. Kuwahi katika vituo vya huduma za afya unapoona dalili za ugonjwa wa Homa ya Nyani.
- viii. Watoa huduma za afya kuzingatia miongozo ya kuzuia kusambaa kwa maambukizi (IPC) wakati wote wanapowahudumia wagonjwa.

Aidha, Wizara ya Afya imejipanga vyema kuhakikisha itatoa huduma bora za matibabu endapo mgonjwa mwenye Homa ya Nyani atagundulika hapa Zanzibar. Wizara inawakaribisha wageni wote kutembelea visiwa vya Zanzibar kwa vile vipo salama.

Ahsateni



**NASSOR AHMED MAZROUI
WAZIRI WA AFYA
ZANZIBAR**